Toleo 49

# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

## NI LAZIMA MZALIWE MARA YA PILI

Huku kukiwa na giza la usiku, Nikodema alifanya juhudi za kumtafuta Yesu. Nikodemo alikuwa mmoja wa Baraza la Sanhedirini, ambalo ndilo lilikuwa linatawala taifa la Wayahudi. Na kwa sababu alikuwa Mfarisayo, yeye aliamini kwamba watu walihitaji kufuata Sheria ya Musa kwa ukamilifu wote. Kwa hivyo hakuna shaka kwamba matembezi haya yake ya kumtafuta Yesu yalifanywa bila mtu yeyote mwingine kujua, kutokana na cheo chake kama kiongozi wa Wayahudi.

Nikodema alimwita Yesu "Mwalimu, Rabi," ambalo lilikuwa jina la heshima la waalimu wa Kiyahudi. Alitambua kwamba Yesu alikuwa ametumwa kutoka kwa Mungu kutokana na miujiza ambayo alikuwa akitenda. Naye Yesu akamjibu Nikodema kwa maneno ambayo yametumika kwa karne nyingi sasa, na ambayo yanatoa changamoto kwa mioyo na fikira za wanadamu kwamba wanahitaji kutafuta kile ambacho ni kikuu zaidi ya kingine chote ambacho wanaweza kupata kwenye ulimwengu huu. "Yesu akajibu, akamwambia, amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu."

Ili mtu apate haki ya kweli, na awe na amani na furaha katika ulimwengu huu, pamoja na kupata uzima wa milele maisha haya yakifika kikomo—zote hizi ni vipawa ambavyo vinapatikana tu katika ufalme wa Mungu—na mtu hawezi kuzipata bila kwanza kuzaliwa tena kiroho. "Kuzaliwa mara ya pili" kunamaanisha mtu kupata mageuzi ya kiroho. Hayo sio mageuzi ya kimwili, bali ni kazi ya kiungu ya Mungu ambayo kupitia kwake Yeye anahuisha nafsi ya mwanadamu.

Kuzaliwa ndio mwanzo wa maisha. Wakati tunapozaliwa kimwili hapo ndipo mwanzo wa maisha yetu ulimwenguni huu, na kuzaliwa huko kwa kiroho kunaashiria mwanzo wa maisha yetu ya kutembea na Bwana. Lakini kuzaliwa huku kwa kiroho hakutokani na mtu kujiunga na kikundi fulani cha kidini, kubadilisha maadili yake, au kuishi kulingana na viwango bora vya tabia, au hata zaidi yeye kufuata kanuni fulani za kumwabudu Mungu. Kuzaliwa mara ya pili ni kazi ya Yesu Kristo. Wakati watu wameweka imani yao katika kifo cha kujitolea cha Yesu Kristo Mwana wa Mungu, pamoja pia na kufufuka kwake, Yeye hutunyooshea msamaha wa dhambi na kutupatanisha tena na Mungu. Tendo hili la kufanywa upya, au kuzaliwa mara ya pili, ni jambo linalofanyika kupitia kwa nguvu za kiungu za Mungu. Yeye huhuisha mioyo yetu na kutufanya viumbe vipya. Nguvu za dhambi huvunjiliwa mbali, na watu waliozaliwa mara ya pili wanaweza kuishi katika uhuru na utakatifu wa Yesu Kristo, ila si kwa nguvu zao wenyewe, bali kutokana na mageuzi ya kiungu ya nafsi zao kupitia kwa nguvu zake Mungu.

Wokovu unambidi mtu kuzaliwa upya kiroho, na bila uzao huo watu huendelea kuwa wafu kiroho na kutenganishwa na Mungu. Ndiposa kufanya ibada misikitini, hekaluni, kwenye Hema, au katika kanisa ndogo hakuwezi kumfanya mtu kuzaliwa mara ya pili. Watu wengi wa kidini bado hawajapata ujuzi huo wa kuzaliwa kiroho ambao Yesu alizungumza kuhusu. Lakini Yeye alimwambia Nikodema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili . . ." Bila kuzingatia cheo (cha mtu) katika jamii au hadhi inayotokana na utajiri wake, urithi wake wa kiroho, utaifa wake, umri wake, jinsia yake, au dhehebu lake; ni lazima watu WOTE wazaliwe tena kiroho ili wapate uzima wa milele. Hata kumtambua Kristo kama Masia hakutoshi. Mageuzi ya hali ya juu ya kuzaliwa upya ni jambo la lazima. Maana ya kuzaliwa "upya" ni "kuzaliwa mara ya pili," na pia linamaanisha "kuzaliwa kutoka juu." Basi kuzaliwa kiroho

*(Endelea katika Ukurasa 2)*



"Wokovu unambidi mtu kuzaliwa upya kiroho, na bila uzao huo watu huendelea kuwa wafu kiroho na kutenganishwa na Mungu."


| Tahariri | Mwongozo wa Kujifunza Biblia: Kuzaliwa Kiroho | Kutoka Kifoni na Kuingia Uzimani | Maswali na Majibu | Je, Wajua? Neno Linalofaa kwa Msimu Huu |
|---|---|---|---|---|
| 3 | 4 | 5-6 | 7 | 8 |

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17

**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11

**Urembo wa Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20

**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)*

sio tu mtu kumkiri Kristo au kukiri dhambi zake, bali ni jambo linalofanyika wakati nafsi ya mwanadamu imegeuzwa na kuweza kutoka dhambini na uchafu wake na anapokea haki na utakatifu. Uzao huu wa kiroho hautokani na bidii za mwanadamu, bali ni uzao wa kiungu katika roho ya mwanadamu, ambao unafanyika mara moja kupitia kwa kitendo cha nguvu zake Mungu.

Watoto wanapozaliwa wao huwa wanarithi vitambulishi na mienendo ya wazazi wao. Vivyo hivyo watu wanapozaliwa upya kitambulisho chao hubadilika na wanafanyika kuwa wana wa Mungu. Kutoka hapo wao huwa hawajafungwa na umwili wao bali wanakuwa washiriki wa asili ya kiungu, huku wakipata nguvu ndani yake Mungu ya kushinda dhambi.

> "Kuzaliwa mara ya pili. . . (sisi) huhuishwa kiroho, tunapewa nafasi nyingine, na tunapata ahadi ya tumaini la milele."

Katika Yohana 3:6 Yesu alimwambia Nikodema, "Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho." Uzao wa kawaida hufuatilia mambo ya kimwili, na kazi zetu pamote na matendo yetu huwa ya kimwili, lakini kuna kuzaliwa kwa aina nyingine. Kile ambacho kimezaliwa na Roho wa Mungu ni cha kiroho. Ni jambo la huzuni kwamba watu wengi hujaribu kukutana na mahitaji ya nafsi zao kwa kufuatilia tamaa zao za dhambi, au kwa kujiunga na vikundi vya wanadamu, au vikundi vya kidini, na pia kwa kufuata falsafa za kibinadamu. Lakini kama ambavyo tulizaliwa katika mwili, HATUNA BUDI kuzaliwa kiroho.

Kuzaliwa mara ya pili ni zaidi ya dhana ya kithiolojia; bali ni mwaliko wa mtu kuweza kupata ujuzi wa maisha yaliyogeuzwa kutoka nje hadi ndani, ujuzi ambao ni mkubwa zaidi ya furaha tunayopata kwa kushiriki katika dhambi, au tunazopata kutoka kwenye dini. Katika kuzaliwa tena sisi huhuishwa kiroho, tunapewa nafasi nyingine, na tunapata ahadi ya tumaini la milele.

Je, wewe umezaliwa mara ya pili? Njia ya PEKEE ya kurithi uzima wa milele ni kupitia kuzaliwa kiroho. Hebu basi fungua moyo wako na kuweka imani yako katika Bwana Yesu kama Mwana wa Mungu. Hebu weka tumaini lako katika kazi ya ukombozi wa Yesu, ambaye alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zako. Hebu ukiri utupu wako wa kiroho, na pia ukiri dhambi zako na kuziacha, huku usiyasalimisha maisha yako kwake Mungu. Hebu mkaribishe Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yako. Utakapofanya hivyo Yeye atafanya muujiza katika maisha yako ya wewe kuzaliwa kiroho, nayo nafsi yako itageuzwe ili itoke kifoni na kuingia kwenye uzima. ■



Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya *www.thegospeltruth.org* na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako. —Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the gospeltruth.org

# Tahariri



*Si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu.* —Tito 3:5

Ni kupitia kwa rehema na upendo wake Mungu ndipo tunaweza kuokolewa. Hakuna hata mmoja wetu ambaye anastahili wokovu, bali ni kipawa cha kiungu chake Mungu. Hakuna haja ya kukazana ili kupewa kipawa, kwa maana kwa asili yake kipawa hutolewa bila malipo. Yesu alikuja duniani na kujitoa kama kafara ili tutakaswe kutokana na dhambi zetu na kuweza kurithi uzima wa milele. Kipawa hiki cha wokovu ni cha thamani kuu kuliko faraja na vito vyote vya ulimwengu huu.

Somo la robo hii ya mwaka, "Kuzaliwa Kiroho," linadhihirisha ukweli mkuu wa kithiolojia na matukio ya kawaida ya mtu kuweza kuzaliwa mara ya pili. Nilipokuwa najifunza kuhusu swala hili kutoka kwa maandiko, nilishangazwe sana kutokana na kutambua urihisi na nguvu za injili.

Kuzaliwa mara ya pili ni jambo ambalo imani na dini nyingi hazielewi maana yake. Dini nyingi hufundisha kwamba kupata ufahamu au kumkubali Mungu ni jambo ambalo linaweza kupatikana kupitia kwa bidii za mtu na kufuata sheria na maagizo. Watu hufanya bidii ili kupata furaha na usalama wa uzima wa milele. Lakini ili mtu aweze kukombolewa kutoka kwa dhambi na kuingia katika Ufalme wa Mungu ambao ni wa ajabu, ni lazima kuwe na mageuzi ya nafsi yake. Muujiza wa wokovu haupatikani kupitia kwa haki yetu wenyewe bali ni kwa kupitia kwa kuzaliwa kiroho. Kwa hivyo hata ingawa kuna miongozo muhimu ya kimaandiko ambayo tunahitaji kufuata, kazi zetu za kutafuta utakatifu wa kimwili haziwezi kutuokoa.

*Tutembelee www.thegospeltruth.org ili kujiandikisha na kupata jarida za mbele.*

Kushiriki katika kanisa, kuwa mshiriki wa kusanyiko fulani, kuishi maisha maadilifu, kuomba, kusoma maandiko, kutoa fedha zako, na kuwatumikia watu wale wengine sio mambo ambayo yanaweza kumletea mtu wokovu. Wokovu unahitaji kazi ya kiungu ya Mungu. Kuzaliwa mara ya pili ni Mungu kufanya maishani mwetu kile ambacho sisi hatuwezi kujifanyia. Watu wote wanahitaji kuzaliwa kiroho. Hata watoto ambao wamezaliwa katika jamii za Kikristo wanahitaji uzao huo wa kiroho, kama ambavyo watoto wa wasioamini wanavyouhitaji.

Mtu akizaliwa kiroho huwa kwamba yeye amegeuzwa. Kuna jambo linalofanyika wakati huo ambalo mara nyingi haliwezi kuelezeka vizuri. Kwa nguvu za Mungu dhambi zake husamehewa, moyo wake unafanywa safi, na nafsi yake inawekwa huru kutokana na laana ya kifo. Hebu basi tumshukuru Mungu kwamba sisi tumezaliwa mara ya pili!

Kuna faraja kuu inayotokana na ujuzi wa mtu kuzaliwa mara ya pili. Hapo ndipo tunanyenyekea kwa mapenzi ya Mungu na kusalimisha maisha yetu kwake, na mtu anapata amani kwa sababu ya kujua kwamba sasa yeye ni mtoto wa Mungu. Kwa kweli tungali tutafanya makosa wakati tunaendelea kukua kama Wakristo, lakini pia tunaweza kuishi bila kutenda dhambi. Tunaweza kupata pumziko katika neema ya wokovu wa Kristo na kwa kujua kwamba tumezaliwa tena—kwamba tuko hai, tumegeuzwa, na tumesamehewa.

Ingawa mimi nafurahia kujua maana ya kuzaliwa kiroho, moyo wangu una majonzi mengi kwa ajili ya watu wale ambao wanafanya juhudi sana ili kustahili wema wa Mungu kupitia kwa bidii zao wenyewe. Bidii zao ni jitihada ambazo haziwezi kumwezesha mtu kupata utakatifu wa kweli. Chochote kingine upatacho bila kupata ujuzi wa kuzaliwa mara ya pili ni kitu ambacho hakifaidi chochote. Utakatifu wa kweli, amani, na furaha ni mambo ambayo yanapatikana kwa mtu tu kuingia ufalme wa Mungu kwa njia ya kuzaliwa kiroho.

Ombi langu ni kwamba ujumbe huu wa watu kuzaliwa kiroho utawafikia wote waliopotea ili uendelee kuyageuza maisha yao.

Michael W. Smith

Julai, 2024



# Mwongozo wa Kujifunza Biblia

## Somo: Kuzaliwa Kiroho

**Masomo ya Maandiko:**
*Yesu akajibu, akamwambia, amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.*
—Yohana 3:3

**Muhtasari:**
Wanadamu wote wako chini ya hukumu ya kifo kutokana na dhambi. Ili mtu aingie katika ufalme wa Mungu inambidi apata uhuisho wa kiroho wa nafsi yake, ambao ni mageuzi yanayoletwa na nguvu za Mungu. Kuzaliwa huku kwa kiroho hutakasa nafsi ya mwanadamu anatoka dhambini na kumpatia nguvu ya kushiriki katika asili ya kiungu.

### I. Kifo cha Kiroho

A. Warumi 5:12 Mauti iliwafikia watu wote.
B. Warumi 3:23-24 Wote wametenda dhambi.
C. Warumi 6:23 Mshahara wa dhambi ni mauti.

### II. Kuokoka

A. Matendo 3:19 Tubuni mrejee.
B. Mathayo 18:3 Msipoongoka.

### III. Kuzaliwa Mara ya Pili

A. Yohana 3:1-8 Mtu asipozaliwa mara ya pili.
B. 1 Petro 1:23 Mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo.

### IV. Kiumbe Kipya

A. 2 Wakorintho 5:17 Kiumbe kipya ndani yake Kristo.
B. Isaya 1:18 Kutakaswa kutokana na dhambi.

### V. Kufanywa Upya

A. Tito 3:5 kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya.
B. Ezekieli 36:24-27 Moyo mpya na roho mpya.

### VI. Kuzaliwa Kiroho Hutokana na Mapenzi ya Mungu

A. Yohana 1:12-13 Haitokani na Mapenzi ya Mtu.
B. Waefeso 2:8-10 Wokovu ni kipawa cha Mungu.

### VII. Ukombozi

A. 1 Petro 1:18-19 Hatujakombolewa kwa vitu.
B. Wagalatia 6:15 Kutahiriwa au kutotahiriwa sio mambo muhimu.

### VIII. Mtu wa Kiroho

A. 2 Wakorintho 4:16 Mtu wa ndani anafanywa upya.
B. Wakolosai 3:9-11 Kuvaa utu mpya.

### IX. Asili ya Kiungu

A. 2 Petro 1:3-4 Washirika wa asili ya kiungu.
B. Waefeso 4:24 Mtu mpya ameumbwa katika utakatifu.
C. Wagalatia 5:19-24 Matendo ya mwili yakilinganishwa na matendo ya Roho.

### X. Ushahidi wa Uzao Mpya

A. 1 Yohana 3:9 Hatendi dhambi.
B. 1 Yohana 5:4 Anashinda ulimwengu.
C. 1 Yohana 2:29 Anatenda haki.

### XI. Kitambulisho na Kukua Katika Kristo

A. Waefeso 3:14-17 Familia imeitwa kwa jina la Baba.
B. Waefeso 4:15 Kukua ndani yake Kristo.

**Tamati**

*(Alituhuisha); Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu.*
—Waefeso 2:1



# Kutoka Kifoni na Kuingia Uzimani

Wakati ulimwengu ulipoumbwa Mungu alimuumba mwanadamu, akampa (sio tu) mwili na nyama, bali pia nafsi isiyofariki. Lakini wanadamu walinajisi nafsi hii kupitia kwa dhambi na wakajiletea laana ya kifo cha kimwili na kiroho. Lakini mambo hayakuishia hapo, Mungu aliunda njia ya kuleta ukombozi, njia ya mtu kuepuka nguvu za dhambi na tangazo hilo la kifo—akaweza kuzaliwa tena kiroho.

"Zaidi ya kuzaliwa kwa asili ya mwanadamu kuna kuzaliwa kwingine kwa kiroho ambako kupitia kwake kunapatikana mabadiliko makuu na kugeuzwa kwa roho ya mwanadamu . . . Mungu anambadilisha mwanadamu huyo ambaye maisha yake yalikuwa yamezoroteka, mtu asiye na haki, na aliyejaa dhambi, na anaweza kuwa safi, mtu asiye na ila, na mwenye uungu.."

## Kufa Dhambini

Hukumu ya kifo ilipitishwa dhidi ya watu wote kutokana na dhambi, ambayo milele ndiyo hutenganisha mwanadamu na Mungu. Warumi 3:23 inatufundisha kwamba, "Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." Lakini kutokana na upendo wake, Mungu alitengeneza njia ambayo iliwawezesha watu aliowaumba kuwekwa huru kutokana na laana ya dhambi na kifo. Ndiposa akamtuma Mwanawe Yesu, pamoja na Roho Mtakatifu, ili kugeuza nafsi ya mwanadamu ili itoke kifoni na kuingia uzimani. "Wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu" (Warumi 3:24). Kutoka katika hali ambayo tulikuwa tumekata tamaa, tukapata tumaini na ahadi ya uzima wa milele kupitia kwa ukombozi wa Mungu na nguvu zake za utakaso. "Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu" (Warumi 6:23).

## Ujumbe wa Tumaini la Injili

Ujumbe mkuu wa injili ni wito wa "Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe" (Matendo 3:19). Kuokolewa huleta mabadiliko makuu, tunabadilishiwa maisha juu chini. Hili ni jambo linalopindua mwenendo wa maisha ya mtu, tabia zake, falsafa zake, na njia zake. Nafsi ambayo haijaratibiwa humwongoza mtu kwenye maangamiza ya milele. Yesu mwenyewe alitangaza, "Msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni" (Mathayo 18:3).

## Tiba ya Dhambi

Tiba ya dhambi ni nini? Mtu anawezaje kugeuka kutoka kwa tamaa za mwili na shauku zake ambazo huongoza mwelekeo wa maisha yake? Jambo hili hulazimu nguvu za kiungu kuingilia kati, kwani inambidi mtu kuzaliwa kiroho. Yesu alimwambia Nikodema katika Yohana 3:3-6, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu . . . kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho." Zaidi ya kuzaliwa kwa asili ya mwanadamu kuna kuzaliwa kwingine kwa kiroho ambako kupitia kwake kunapatikana mabadiliko makuu na kugeuzwa kwa roho ya mwanadamu. Kuzaliwa kiroho kunafungua muujiza wa maisha kama ambavyo uzao wa kiasili unavyofanya. Mungu anambadilisha mwanadamu huyo ambaye maisha yake yalikuwa yamezoroteka, mtu asiye na haki, na aliyejaa dhambi, na anaweza kuwa safi, mtu asiye na ila, na mwenye uungu. Katika 1 Petro 1:23 mtume Petro anasema kuhusu uzao huu, "Mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele." Kuzaliwa huku kwa kiroho hakutokani na familia ulikozaliwa, uzao ule ambao mwisho wake huwa ni kifo, bali unatokana na Neno la Mungu, ambalo humpa mtu uzima.

## Muujiza wa Wokovu

Mtu akimkubali Yesu Kristo kama mwokozi, Mungu hufanya muujiza wa kuyageuza maisha yake. "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya" (2 Wakorintho 5:17). Nguvu za dhambi zinavunjwa na mtu anarudishiwa hali ya kutokuwa na hatia, anakuwa mtu safi kwa njia ya kuzaliwa kiroho. Muumini huyu haendelei kudumu katika dhambi ila anatawala juu ya dhambi kupitia kwa nguvu za uzao mpya. Nabii Isaya alieleza utakaso ambao mtu hupata katika ujuzi huu kwa maneno yafuatayo: "Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu" (Isaya 1:18). Mungu huosha na kutakasa nafsi ya mwanadamu katika kuzaliwa huku kwa kiroho.

## Kuzaliwa Kiroho

Maandiko huita kuzaliwa huku kwa kiroho kuwa kuzaliwa kwa pili, tendo la kufanywa upya, tendo la kuzaliwa tena.

*(Endelea katika Ukurasa 6)*

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 5)*

"Si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu" (Tito 3:5). Mpango kamili wa ukombozi na wokovu unahusisha kutakaswa kwa nafsi ya mwanadamu kutokana na dhambi, na kujazwa na Roho Mtakatifu. Hii husababisha kuzaliwa upya kwa nafsi ya mwanadamu. Nabii Ezekieli alitabiri kuhusu ujuzi huu wa ajabu: "Nami nitawanyunyizia maji safi, nanyi mtakuwa safi; nitawatakaseni na uchafu wenu wote, na vinyago vyenu vyote. Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama. Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda" (Ezekieli 36:25-27). Mungu asifiwe sana! Bwana anatutakasa kwa damu yake na kwa maji ya Neno lake. Anatuondolea moyo mgumu (wa kale) uliojaa dhambi, na kuweka Roho wake ndani yetu. Uzao huu mpya wa kiroho unatupatia nguvu ya kufuata njia za Bwana na kuishi maisha ya utakatifu.



"Hata ingawa sisi tungali tuko na nguvu pamoja na udhaifu wa maumbile yetu ya kawaida, baada ya nafsi zetu kuokolewa, tunapata nguvu pamoja na Mungu ya kukabiliana na dhambi za maadili ambazo mwanzoni zilitutenganisha na Mungu.."

## Wokovu Hutoka kwa Mungu Peke Yake

Ingawa ni lazima mtu awe tayari kufungua moyo wake kwa Mungu kwa hiari yake, ili kuweza kupata mageuzi hayo ya kiroho, hakuna uamuzi wa kibinadamu au kusudi la mtu peke yake ambao unaweza kumletea mwenye dhambi mageuzi hayo ya kutoka katika maisha ya dhambi. Uzao mpya wa kiroho hutoka kwa Mungu peke yake, si kupitia urithi wake wa kiroho au utaifa wake. Kama ambavyo Yohana 1:12-13 inavyosema, wale ambao wanafanyika watoto wa Mungu hufanyika "si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu." Mtu hawezi kustahili wokovu kwa kuufanyia kazi au kwa bidii za kibinadamu. "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu" (Waefeso 2:8-9).

## Haupatikani kwa Kufanya Kazi

Watu wengi hutafuta maisha ya kiroho na ukombozi kupitia kwa matendo yao, matendo yao ya wema, na kwa wao kuwa waadilifu, au kupitia kwa dini zao. Lakini uzima wa kweli na utakatifu hupatikana kupitia kazi ya kiungu ya Mungu peke yake. "Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani . . . ya Kristo" (1 Petro 1:18-19). Kuabudu, kufanya matambiko, kufuata tamaduni, au hata kuishi maisha ya viwango vya juu vya maadili sio mambo yanaweza kumfanya mtu akubalike machoni pake Mungu. Ukombozi ni jambo ambalo haliwezi kupatikana kwa bidii za mwanadamu; inachukua nguvu za Muumbaji kuanzisha uzao huo mpya wa kiroho.

## Mtu wa Kiroho

Mwanadamu hudumu kama kiumbe cha kimwili na kiroho. Hata ingawa mtu wa nje ataangamia kwa njia ya ugonjwa na kifo, "utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku" (2 Wakorintho 4:16). Mtume Paulo anamtaja mtu wa kiroho katika Wakolosai 3:9-10 "Mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake; mkivaa utu mpya, unaofanywa upya upate ufahamu sawasawa na mfano wake yeye aliyeuumba." Mtu wetu wa kale wa dhambi hubadilishwa na kuwa mtu mpya, mtu ambaye ameumbwa kwa mfano wake Mungu.

## Washiriki wa Asili ya Kiungu

Kusudi la wokovu ni kuwatoa watu katika hali ya kuwa na dhambi, na kuwafikisha katika hali ya usafi. Kuzaliwa huku kwa kiroho huleta mabadiliko makubwa katika asili na mwelekeo wa mwanadamu. "Ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa" (2 Petro 1:3-4). Kwa hivyo hata ingawa tungali tunazo tamaa za kibinadamu na majaribu, tunapata mageuzi ya tabia zetu za maadili. Waefeso 4:24 inatupatia mwongozo kwamba "Mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli."

## Ushahidi wa Uzao Mpya

Hata ingawa sisi tungali tuko na nguvu pamoja na udhaifu wa maumbile yetu ya kawaida, baada ya nafsi zetu kuokolewa, tunapata nguvu pamoja na Mungu ya kukabiliana na dhambi za maadili ambazo mwanzoni zilitutenganisha na Mungu. Ushahidi wa uzao huo mpya umedokezwa katika Yohana wa Kwanza: "Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi" (3:9); "Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu" (5:4); "Kama mkijua ya kuwa yeye ni mwenye haki, jueni ya kuwa kila atendaye haki amezaliwa na yeye" (2:29). Maandiko haya yanaonyesha jinsi maisha yetu hubadilishwa kwa hali ya juu katika vipengee vya maadili na kiroho.

## Kitambulisho na Kukua Katika Kristo

Kama watoto waliozaliwa kwa njia ya kawaida tunapata kitambulisho na maumbile ya asili ya wazazi wetu, na hivyo ndivyo ilivyo kwa wale waliozaliwa mara ya pili. Waefeso 3:15 inasema familia yote ya mbingu na nchi imeitwa kwa jina la Baba. Kama Wakristo waliozaliwa mara ya pili tunajitambulisha na Mungu; na shauku zetu hulingana na mapenzi yake Mungu. Kama ambavyo mtoto mchanga anavyokua na kukomaa, hivyo ndivyo ilivyo kwa mtu ambaye amezaliwa kiroho. "Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo." Lakini hata ingawa kukua huku huendelea katika safari yetu yote ya maisha, hakuna baraka zingine za hali ya juu zaidi kushinda zile tunapata kutokana na ujuzi wa kuzaliwa mara ya pili (Waefeso 4:15) . ■

# Maswali na Majibu

## Je, katika Yohana 3:5 ni nini maana ya "kuzaliwa kwa maji?"

Katika Yohana 3 mazungumzo kati ya Yesu na Nikodema kuhusu kuzaliwa mara ya pili yalihusisha maneno yafuatayo, "Mtu asipozaliwa qkwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu." Neno 'maji' hapa likitazamwa kithiolojia huwa kwamba halieleweki vizuri, na watu wengine wanalitafsiri kwa njia tofauti tofauti.

Usemi huu ulisemwa na Yesu baada ya Nikodema kuuliza kuhusu mtu kuingia mara ya pili kwenye tumbo la mamake ili azaliwe tena. Kuna tafsiri za aina tatu za msemo huu ambazo nitaziangalia kwa kifupi.

**1. Kwamba ni Kuzaliwa Kimwili:** "Kuzaliwa kwa maji" kunaweza kuwa ni maneno ambayo yananena kuhusu kuzaliwa kimwili. Kuzaliwa kwa kwanza ni kuzaliwa ambako hutokana na maji (yaani majimaji ya amniotic fluid), na kuzaliwa mara ya pili ni kule kuzaliwa kwa roho ya mwanadamu kwa njia ya kiroho. Yesu anazilinganisha semi hizo mbili hivi: "Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho." Usemi huu unatenganisha mambo ya kimwili kutokana na mambo ya kiroho.

**2. Kwamba ni Mfano wa Kuoshwa:** Katika Maandiko maji mara nyingi hutumiwa kuwakilisha utakaso na kusafishwa. Waefeso 5:26 inasema kuhusu Kristo akiosha kanisa ili "alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno." Nayo Ezekieli 36:25-27 inasema "Nami nitawanyunyizia maji safi, nanyi mtakuwa safi; . . . nami nitatia roho yangu ndani yenu." Matumizi ya 'maji' na 'roho' kama inavyoonekana katika Yohana 3:5 inaweza kuashiria kweli ambazo ni za kiroho. Yesu alisema katika Yohana 15:3 "Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno . . ." Naye Mtume Paulo alisema kwamba Wakristo "wameoshwa" (1 Wakorintho 6:11). Kuzaliwa mara ya pili ni kuzaliwa kutoka juu, jambo ambalo linaweza kuwa linaonyesha kwamba maji na roho ambazo zinazungumziwa hapa ni vitu vya asili ya kiroho, ambavyo Mungu angetumia ili kuwaosha watu. Basi ujuzi wa kuzaliwa mara ya pili ungemfikia mwanadamu kwa njia ya utakaso kwa kutumia Neno la Mungu pamoja na Roho wake.

**3. Pia Yanatumiwa Kutafsiri Ubatizo kwa Njia Ambayo Haifai:** Maoni ya tatu ambayo hayako sahihi husema kwamba "kuzaliwa kwa maji" ni kitu kinacholingana na ubatizo wa Kikristo, na hivyo kujaribu kuonyesha kwamba ubatizo ni jambo la lazima ili mtu kuweza kupata wokovu. Lakini wazo hili liko kinyume na kanuni na ukweli kwamba wokovu ni tendo la kiungu, na sio kazi ya kibinadamu. Kulingana na maandiko ubatizo ni kazi ya kibinadamu inayofanywa kwa njia inayoonekana na inakuwa ushuhuda wa kazi ya kindani ya Mungu. Mwizi yule ambaye alikuwa msalabani pamoja na Yesu hakuwa amebatizwa, lakini aliahidiwa kwamba atafika paradiso, na yeye akawa dhibitisho kwamba swala hili la "kuzaliwa kwa maji" halisemi kuhusu ubatizo wa maji.

# Hatua 5 za Mtu Kupata Wokovu

Kuzaliwa kiroho ni kazi ya kiungu ya Mungu katika nafsi ya mwanadamu. Lakini hata ingawa kazi hii haifanyiki kupitia kwa bidii zetu, ni lazima tutimize masharti kadhaa ili Mungu aweze kutupatia mageuzi hayo ya ajabu. "Wokovu hutoka kwa BWANA" (Yona 2:9).

### Kuisikia Injili

Warumi 10:17 Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.

### Kumwamini Yesu kama Mwana wa Mungu

Yohana 3:16 Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele

### Kumwita Mungu

Warumi 10:13 Kwa kuwa, kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka.

### Kukiri

1 Yohana 1:9 Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.

### Kukiri Dhambi

Matendo 3:19 Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana.

JE, WAJUA?

Nikodema, ambaye alikuwa Mfarisayo, ametajwa tu katika Injili ya Yohana. Kusema kweli yeye hajatajwa katika Injili ingine. Hadithi yake inasimuliwa katika matukio matatu makuu:

1. Mazungumzo yake ya hali ya juu pamoja na Yesu kuhusiana na swala la kuzaliwa kiroho (Yohana 3:1-21).

2. Kumtetea Yesu wakati Nikodema alisisitiza kufanywe kesi ya haki ambayo ililingana na sheria dhidi yake Yesu wakati walimfanyia kesi katika Baraza la Sanhedrin (Yohana 7:50-51).

3. Tendo lake la kujitolea kumtumikia Yesu wakati yeye na Yohana wa Arimathea walipopaka mwili wa Yesu manemane na uudi na baadaye kuzika mwili huo kwenye kaburi (Yohana 19:38-42).

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

# KUWABARIKI WATOTO WA MUNGU

*Nena na Haruni na wanawe, uwaambie, hivi ndivyo mtakavyowabarikia wana wa Israeli.*
—Hesabu 6:23

Mungu alimpatia Musa mwongozo wa jinsi kuhani mkuu Haruni angetangaza baraka kubwa juu ya wana wa Israeli. Ombi hili la baraka na lenye ufasaha mwingi linadhihirisha nia ya ndani kabisa ya moyo wa Mungu:

> BWANA akubarikie, na kukulinda; BWANA akuangazie nuru za uso wake, na kukufadhili; BWANA akuinulie uso wake, na kukupa amani (mstari wa 24-26).

Shauku la Mungu la kubariki watoto wake halijabadilika. Baraka za kweli zinatoka kwa Mungu Muumbaji. Baraka hii ilikuwa ni tangazo la kile ambacho Mungu angali anataka kuwafanyia watoto wake hadi leo.

Wokovu hauwaweki watu huru dhidi ya majaribu na mambo mengine magumu. Wakati mwingine mioyo yetu itakuwa na machozi kwa sababu ya mizigo mizito ambayo maisha haya yametuletea. Katika nyakati kama hizo, hebu tuinue macho yetu na kuona zaidi ya shida tulizo nazo na kumgeukia Bwana wetu. Hebu tukumbuke kwamba moyo wake huguzwa na mambo yanayotulemea. Hebu basi tusikilize sauti ndogo iliyojaa utulivu ya Roho wa Mungu akitupatia hakikisho kwamba:

> Nitakubariki. Nitakuweka salama na niwe kimbilio lako katika mawimbi. Nitakutunza na kukuongoza kwa mwangaza wangu. Nitakuwa mpole kwako na kukwonyesha rehema. Nitakufunika na uwepo wangu na kukupa amani.

Usemi huu ni zaidi ya shairi, kwa sababu hii ndio baraka ambayo Mungu huwabariki watoto wake. Wakati vichwa vyetu vimeinamishwa huku mizigo mizito imegandamiza mioyo yetu, tunaweza kukumbuka shauku lake Mungu la kutaka kutubariki. Na huku tukishapata nguvu za kindani, na kujazwa amani ya Mungu, na kufunikwa na rehema zake, pamoja na kukumbutiwa na upendo wake Mungu, tutapata nguvu za kuweza kushiriki baraka hii kwa watu wale wengine ulimwenguni.

Tunaweza kuwahakikishia wenzetu kuhusu upendo na faraja yake Mungu, na pia tunaweza kuwabariki, kama vile ambavyo Haruni aliwabariki wana wa Israeli kwa jina lake Bwana. Sisi hatuko peko yetu; hatujaachwa bila faraja. Badala yake tunaweza kuinuka kwa nguvu kutokana na neema yake Mungu, huku tukiwa tayari kutumika kama vyombo vya kupitisha baraka zake Mungu.

Hebu basi tusonge na kushiriki amani hiyo ambayo imezidi ufahamu, upendo huo ambao hauna mipaka, na faraja ambayo humdumisha mtu hata katika nyakati zilizojaa giza totoro. Hebu tuwe watu wanaopitisha neema ya Mungu ili iwafikia watu wale wengine, huku mwanga wa uso wake uking'ara juu yetu wakati tukienenda kwa nguvu zake Mungu. ■

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

Utakatifu kwa Bwana